# MTIHANI WA www.freekcsepastpapers.com KIDATO CHA KWANZA-2016

**KISWAHILI KIDATO CHA KWANZA**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA**

**MARCH/APRIL**

**MUDA:SAA 2 ½**

**Jina:………………………………………………...Nambari ya Usajili……………………………..**

**Shule………………………………………….**

**Maagizo:**

**1.** Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

**Kwa matumizi ya mtihani pekee.**

| **Swali** | **Upeo** | **Alama** |
|---|---|---|
| **1** | **20** | |
| **2** | **20** | |
| **3** | **40** | |
| **4** | **10** | |
| **Jumla** | **90** | |

**1. UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Nairobi, mji mkuu wa Kenya ,ni jiji Ia maajabu na mastaajabu chungu nzima.Nadhari ya mtu anayewahi kuingia jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo msheheneko wa majumba ya fahari, marefu ajabu ,kiasi chaminazi mitano-sita ,iliyounganishwa kuelekea juu. mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile Ia makongamano ya kimataifa Iiitwalo kwa Kiingereza Kenyatta International Conference Centre Jumba hili,hadi miaka michache iliyopita, ndilo lililokuwa refu zaidi mjini Jumba lenyewe- lina ghorofa ishirini na tisa hivi ,usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake,linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo ,miaka michache iliyopita jengo hili lilipitwa urefu na Mnara wa Nyakati (Times Tower).Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu.Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na majumba haya mawili ,kuna majumba mengine zaidi ya ishirini katikati ya jiji ambayo ,japo mengine ni mafupi kiasi ,yana maumbo ya kustaajabisha kweli kweli.Hebu zingatia mwenyewe jumba Iiitwalo “mdomo wa kengele” au “bell —bottom” ambalo ni vioo vitupu ,toka chini hadi juu.Fauka ya ,umbo lake ni Ia kipekee ulimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo.Linapaa juu ,mbali sana ,likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini;umbo Ia fua pana kama kengele.

Halafu rudia barabara .hizi hazina hesabu katikati ya jiji na ni pana, tena safi sana.Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho,ya kila ama yanashindania nafasi,

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu.Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi ,lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba ,hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi ,kwenda kula chakula cha mchana ,kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyangana .Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi ni wengi kama chungu ,au kama mchanga wa ufuo wa bahari, hatii chumvi.

Watu wa Nairobi ,kwa tabia na mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya .Watu hawa huvalia nadhifu sana.Wanawake ni warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithiIi ya hurulaini peponi.Wengi huvaa suruali ndefu. Kucha zao na midomo yao hupaka rangi maridadi sana.Huzungumza Kiswahili na Kiingereza takriban wakati wote.Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe ,jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini ,hasa kama ulilelewa ukidhani maskani mwafaka ya wanawake ni jikoni peke yake;yaani kuzingatia ile falsafa kuwa “kuoa ni kupata jiko”.Wanaume nao huvaa suti safi ,maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao.Wanaume hao huendesha magari na kuyaegesha karibu na afisi zao.Huingia afisini mwao kwa maringo na madaha,huku funguo za magari yao zikining’inia vidoleni. Hawa nao husema na Kiingereza kupitia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine ,watoto ni nadhifu kweli kweli hasa watoto wa shule.Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyoshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume ,shingoni huvalia tai Watoto wa shule za Nairobi huongea Kiswahili, Kiingereza na sheng,ambayo ni “lahja” yao waliyoibuni.”Lahja” hii ni mchanganyiko wa Kiswahili,Kingereza na msamiati mchache wa lugha nyingine za Wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa jumla ,watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana.Hawana hata wakati wa kutembea polepole na kuangazaangaza huku na huko.lwapo wewe ni mgeni jijini,ukizubaa utapigwa kumbo na <u>waendelee na hamsini zao</u> kama vile hapakutokea jambo.Hili linapojiri, usidhani limefanywa maksudi.La, hasha.Ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

**<u>Maswali</u>**

(a) Kwa nini majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za Kiingereza? (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) (i) Baadhi ya maajabu ya Nairobi ni barabara safi, msongamano wa magari na majumba marefu. Ongezea maajabu mengine matatu. (ala 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli, Fafanua (ala 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) (i) Je, Unadhani watu wa Nairobi kweli hukanyagana? Eleza ni kwa nini msimulizi ametoa maelezo hayo (ala 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanawake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Kwa nini neno “lahja” limewekwa alama za mtajo? (ala 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali za usemi zifuatazo. (ala 3)

(i) Nadhari

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Linaloafiki

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iii) Waendelee na hamsini zao

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

## 2. UFUPISHO

Kiswahili nchini Kenya kilisambazwa kwa njia ya biashara kutoka upwa wa Kenya kwenda bara yake ,ingawa si kwa wingi sana kwa sababu wenyeji wa upwa wa Kenya —Mombasa, Siu na Pate- walikuwa katika vita vya kupigana na utawala wa Kisultani wa Seyyid Said, Sayyid Majid na Seyyid Barrgash.Hata hivyo kuna baadhi ya misafara iliyokwenda bara na kueneza Kiswahili.Kwa mfano, Waswahili wa kutoka Jomvu na Mvita walifanya biashara na Wakamba.Baadhi yao walioa Ukambani na mpaka wa leo kuna milango ya Waswahili ambao nyanya zao wanatoka Ukambani.Wafanyabiashara wengine Waswahili walifika mpaka Umaasaini.

Utawala wa kikoloni ulikitweza sana Kiswahili. Waingereza walitilia mkazo utumiaji wa lugha za kikabila kwa vile walisema kwamba mtu angeeleza hisia zake vizuri kwa kutumia lugha yake ya kwanza.Kiswahili kilitwezwa na kuchukuliwa kuwa ni lugha ya maboi.Wajerumani walikitweza sana nchini Kenya.Wamisheni pia walikipinga Kiswahili kwa sababu ya ufungamanao na Uislamu,

Hata hivyo, Kiswahili kilikuwa kinatumika katika mawasiliano, kwa hivyo wakakata shauri kwamba kitumike katika kufundashia shuleni.Lugha za makabila zilitumiwa katika madarasa ya chini- Kiswahili katika madarasa ya kati, na Kiingereza katika madarasa ya juu.Mtihani wa Kenya African Preliminary Examination (KAPE), ulikuwa ukifanywa katika lugha ya Kswahili nchini Kenya, uliondolewa,

Kiswahili kilitumika katika kuwaunganisha wakenya katika shughuli za ukombozi wa nchi na pia kama lugha ya umma.Mnamo mwaka wa 1964,Tume ya Ominde ilipendekeza kwamba Kiswahili kitumike kwa vile ndiyo lugha ya kumuunganisha Mwafrika, na pia ingetuwezesha kuwasiliana na nchi zingine za Afrika Mashariki na Kongo,

Mnamo mwaka wa 1969, chama cha Kenya National Africa Union (KANU) ,kilifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa, Raisi wa kwanza wa KANU alikuwa akitolea hotuba zake nyingi katika lugha ya Kiswahili, na alitoa kwa Kiingereza kwa ajili ya mabalozi tu.Fasihi ya Kiswahili ilianzishwa mwaka wa 1973, na kwa hivyo wanafunzi wakaanza kuifanya katika kidato cha nne na cha sita.

Ingawa Kiswahili kilitwezwa sana na Waingereza, bado kinatumika na watu wengi kama lugha ya mawasiliano.Mwaka wa 1968, Berndt Heine alifanya uchunguzi na aliona kwamba asilimia 85.25 ya Wakenya hutumia Kiswahili kama lugha yao ya pili na ndiyo lugha ya mawasiliano.Hivi sasa lugha ya Kiswahili imepewa kipaumbele;ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi.Katika sekta ya elimu,Kiswahili ni somo Ia lazima katika shule za msimgi na za sekondari.Ni somo ambalo linanaendeelezwa hata katika vyuo vikuu vya Kenya.

Ni muhimu kutaja kuwa Kiswahili hakikuenea katika bara ya Kenya kama kilivyoenea Tanganyika. Kiswahili kilienea sana Tanzania kwa sababu ya wakoloni, yaani Wajerumani,waliosisitiza matumizi ya Kiswahili;lakini Waingereza walikitweza katika nchi ya Kenya

Licha ya hayo,nchi ya Tanzania ina lugha 120, na Kenya ina lugha kama 41.Nchi ikiwa na lugha nyingi na watu wachache wanaoitumia kila mojawapo ya lugha hizi,ni rahisi kukuza au kuinua lugha moja kuwa lugha ya taifa inayotumiwa na watu wengi.Hoja hii ilifanya Kiswahili kisienee sana Uganda na Kenya ,lakini kikaenea sana Tanzania.

Kiswahili hakikuenea sana nchi ya Kenya kwa sababu biashara haikufana sana katika pwani ya Kenya kama mji wa Unguja.Wanyamwezi na Wayao waliokuwa wakishughulika na biashara huko Tanzania walieneza Kiswahili katika bara, jambo ambalo Wakamba walioshughulika na biashara Kenya hawakushughulika nalo.Wakamba hawakuiga lugha ya watu wa pwani,Wamaasai waliogopwa sana na wafanyabiashara,na kwa hivyo biashara haikufana sana.

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa fupisha aya ya kwanza na ya pili (maneno 50-60) (ala 7)

Nakala chafu

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

Nakala safi

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

(b) Kwa kuzingatia aya za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi (maneno 60 – 70) (ala 8)

Nakala chafu

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………….

Nakala safi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

## MATUMIZI YA LUGHA

**(a)** (i) Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ (ala 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Toa kigezo chochote kimoja cha kuainishia konsonanti. (ala 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(b) Sentensi ifuatayo ina maana mbili tofauti. Zieleze. (ala 2)

Huyu amekuja kutuliza.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) Ikanushe sentensi ifuatayo kwa udogo. (ala 2)

Nyumba yenyewe ilijengwa bondeni karibu na mto.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo: (ala 2)

(i) Mbono (mti)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Barabara (sawasawa)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e) Andika sentensi kuonyesha matumizi mawili ya:

(i) Kinyota (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Ritifaa . (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(f) Tunga sentensi mbili tofauti zinazobainisha maana tofauti kati ya (ala 2)

(i) Nduni

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Duni

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(g) Taja aina zozote mbili za sentensi. (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(h) Andika sentensi ifuatayo iwe katika hai ya -ki- ya masharti (ala 2)

Tulilala sana tukachelewa kwenda shuleni.

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

(i) (1) Taja aina nne za nomino. (al2)

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

(2)Tambua aina za vihusishi vilivyo pigwa mistari katika sentensi zifuatazo. (al2)

(a)Hassan anacheza vizuri **kuliko** Kiprini.

.......................................................................................................................
……………………………………………………………………………………….

(b)Simtambui **kwa vile** amebadilisha nguo.

…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

(j) Taja ngeli za nomino zifuatazo (ala 3)

(1)Ujinga

………………………………………………………………………………………………….

(2)Ugonjwa

………………………………………………………………………………………………..

(3)Kucheza

…………………………………………………………………………………………………

(4)Sukari

…………………………………………………………………………………………………

(5)Barua

…………………………………………………………………………………………………

(6)Mti

…………………………………………………………………………………………………

(k) Tunga sentensi ukitumia nomino ifuatayo pamoja na kivumishi kisisitizi cha mbali kidogo,

Mgomba (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(l) Tunga sentensi mbili ukitumia neno kisabuni kama: (ala 2)

(i ) Nomino

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) kielezi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(m) Andika visawe vya (ala 2)

(i) Hidaya

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Ngeu

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(n) Iandike sentensi ifuatayo upya ukitumia ‘0” rejeshi tamati (ala 2)

Chumvi iliyochafuka si ile unayoizungumzia.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(o) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo (ala 2)

Mwanasiasa shupavu aliyewachochea wananchi amekamatwa.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(p) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja (ala 2)

Nyuzi zisingekatika zisingepotea.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(q) Taja matumizi ya kiambishi ku_ (ala 1)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(r) Taja aina mbili za mofimu (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

4. **ISIMU JAMII**

a. Taja sababu mbili zinazomfanya mzungumzaji kutumia zaidi ya lugha moja katika mazungumzo (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

b. Kwa kutoa mfano, eleza maana ya uwingi lugha. (ala 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

c. Fafanua mambo sita yanaoweza kuifanya lugha yeyote ife, (ala 6)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………